


Kwa miezi mingi anga
lilikuwa kavu.
Lomongin, mbuni
mvua maarufu,
alizungumza na
miungu.

Watu walikusanyika nje
ya boma lake.
Walingoja kwa hamu
na ghamu ujumbe wa
matumaini.



Aliwahakikishia watu
kwamba muumba
angewapa mvua hivi
karibuni.

Wangepanda mimea
yao.




Watoto walicheza nje tulipokuwa tukingoja mvua.

Baadaye siku hiyo, tuliyaona mawingu meupe mbali mashariki. Nilijua ni mawingu ya mvua.




Watu walikuwa bado wanawaza kuhusu kile mbuni mvua alisema.

Mama alipiga yowe kwa sauti, "Pale! Sasa mawingu ni meusi. Njooni ndani."




Mvua ilinyesha.

Ikanyesha!



Tulikuwa tumeingoja
mvua kwa siku nyingi!

Mwanzo, tulifurahi.



Maji yalizidi kuwa kila mahali.

Daraja la kuunganisha kijiji chetu na sehemu nyingine, lilisombwa na maji.



Nyumba zilisombwa na
gharika.

Kile kilikuwa baraka,
kilikuwa sasa ni mauti
kwetu.



Tulikuwa
tumejitayarisha kwa
upanzi, lakini sasa
hatungepanda.
Tulikuwa tumeitamani
mvua, lakini sasa
hatukuitaka tena.

Hatukuwa na daraja la
kuvukia. Wengi
hawakuwa na makazi
wala miji.



Na tulikuwa na shida
nyingine! Tuliona
mamba wakiogelea
kila mahali.

Hili halikuwa limewahi
kutokea tena.

Tulichanganyikiwa!



Hatungeenda
manunuzi kwa sababu
maduka yote yalikuwa
ng'ambo ya mto.

Watoto hawangeenda
shuleni kwa sababu
shule zilikuwa
ng'ambo ya mto.



Kile kingekuwa baraka,
kiligeuka kuwa laana
kwetu. Lomongin,
mbuni mvua, akakata
tamaa vilevile.

Aliyekuwa na furaha
pekee ni Kapuus na
paka wake wanane!